# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.25. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Juni 1-10, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 11-20, 2023*



**MUHTASARI**

- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi yanayopata mvua za Msimu inatarajiwa kusaidia kukomaa kwa mazao hususan mahindi na mpunga na pia kusaidia shughuli za uvunaji wa mazao.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo yanayopata mvua za masika inaweza kuathiri ukuaji wa mahindi yaliyo kwenye hatua ya kukomaa
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani na kutumia taarifa za hali ya hewa katika shughuli zao za kila siku.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2023


Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu. Hali hii iliendelea kuuruhusu Ukanda Mvua (ITCZ) kuambaa nje ya nchi.

Joto la bahari katika eneo la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani, na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kusafirisha hewa yenye unyevunyevu kuelekea ukanda wa pwani ya nchi. Katika eneo la tropiki ya kati ya bahari ya Pasifiki joto la bahari lilikua la wastani hadi juu kidogo ya wastani.

Kwa upande mwingine, joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) lilikua la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2023

Katika kipindi hiki maeneo mengi nchini yalikuwa makavu wakati maeneo machache yalipata mvua chini ya 20 mm. Hata hivyo maeneo machache ya mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua zaidi ya 100 mm kama inavyoonekana katika Kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Juni 1-10, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2023

Mvua zilizonyesha katika dekadi hii, zimesaidia ukuaji na maendeleo ya mazao katika maeneo yanayopata mvua za masika hususan katika maeneo ya ukanda wa pwani ya kaskazini. Hata hivyo, mvua hizo zimesababisha kujaa maji na kuathiri zao la mpunga lililokomaa hususan katika mkoa wa Pwani.

Maeneo yanayopata mvua za masika hususan katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Kagera, Morogoro, Arusha, na Pwani, mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa.

Hali ya ukavu iliyojitokeza hususan katika maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka ilisaidia kukomaa kwa mazao ya mahindi na mpunga yaliyopandwa kwa kuchelewa. Hali hii pia ilisaidia shughuli za uvunaji wa mpunga na uhifadhi.

Kwa ujumla, mazao ya mahindi na mpunga yapo katika hali nzuri hususan kwenye maeneo yanayopata mvua za Msimu.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vilikuwa katika hali ya kawaida katika maeneo mengi nchini.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Dikadi hii migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kidogo wakati ile iliyopo katika kaskazini mwa dunia ikipungua nguvu. Hali ambayo inatarajiwa kuongeza kidogo kasi ya upepo katika maeneo ya mwambao wa pwani hususani katika nusu ya pili ya dekadi.

Joto la bahari katika eneo kubwa la bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu kidogo ya wastani, na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka baharini kuelekea maeneo ya pwani.

Joto la bahari katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusafirisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Maeneo ya kanda ya kanda ya Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kupata mvua na ngurumo zitakazoambatana na radi.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa makavu na yenye vipindi vifupi vya mvua nyepesi hususani katika nusu ya pili ya dekad.

Maeneo ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika maeneno yanayopata mvua za Msimu itasaidia katika kukomaa kwa mahindi pamoja na shughuli za uvunaji zinazoendelea.

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo pwani ya kaskazini na ukanda wa Ziwa Victoria zinatarajiwa kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao hususan mahindi ambayo yapo katika hatua ya kukomaa.

Wakulima na maafisa ugani wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao mashambani ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kutokana na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Jamii za wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye baharini ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Wafugaji pia wanashauriwa kuhakikisha mifugo yao inalindwa dhidi ya hali mbaya ya hewa na magonjwa.

Kwa ujumla, inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa katika shughuli na mipango ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 11-20, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuwa cha kawaida. Hata hivyo, jamii katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua inashauriwa kuvuna maji ya mvua kadiri inavyowezekana kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Na kwa jamii iliyopo maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka inashauriwa kutumia maji yaliyopo kwa uangalifu kufuatia kuanza kwa msimu wa ukavu.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)